

Pambazuko

Toleo Namba 072

Jumatatu Mei 13-19, 2024



**Mifumo ya
elimu
Tanzania
bado kizungumkuti**

UK. 6-7



Jicho la Tai

Samia ashinde huu UK. 5
mtihani wa Muungano

**Malima aumizwa utalii
Morogoro kuwa gizani**



UK.8

**Kondomu
zenye miiba
'kiboko' ya
wabakaji
zaja** UK. 14



**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye
namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

Tahariri

REA ionyeshe mapana ya majukumu yake

WAKATI tukiipongeza serikali kwa kuanzisha mpango wa matumizi ya nishati salama kama njia ya kutunza mazingira na kuimarisha afya, tungependa pia kukumbusha Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kuwa huu ni wakati muafaka kupanua utekelezaji wa majukumu yake ili kutoa taswira halisi ya mawanda ya majukumu yake.

Tangu kuanzishwa kwake, REA imejikita zaidi kusambaza umeme vijijini, kiasi cha watu wengi kuiona taswira pana ya taasisi hiyo kama chombo kinachoshughulikia masuala ya umeme peke yake.

Lakini ikiangaliwa jina la taasisi hiyo, umeme ni sehemu ndogo tu ya mambo ambayo REA inapaswa kuyafanya.

Inawezakana kuwa REA ilijikita zaidi kwenye umeme kwa sababu katika kipindi cha miaka michache iliyopita, mwelekeo wa nchi katika suala la kusambaza umeme, ndilo lililokuwa limepewa kipaumbele.

Hata kama hali ilikuwa hivyo, REA haikupaswa kujiweka kwenye suala hilo la umeme peke yake na kusahau kabisa masuala mengine yanayohusiana na nishati, kwani nayo yapo chini ya majukuu yake.

Sasa wakati ambapo serikali imegeukia suala la nishati salama ya kupikia, ni fursa nzuri sana kwa REA kurudi kwenye mstari na kuonyesha mawanda ya majukumu yake kwa kuliweka suala hilo katika vipaumbele vyake vya utekelezaji.

Wakati serikali ilipokuwa inatekeleza usambazaji wa umeme

vijijini, REA ilionekana ikiongoza katika eneo hilo, lakini ikasahau kushughulika kwa undani na aina nyingine za nishati.

Sasa serikali inapoingia kwenye suala la nishati safi ya kupikia, ni wakati wa REA kujikita huko nako, ingawa safari hii isijisahau kuhusu mawanda na upana wa suala la nishati.

Isishughulike na nishati safi tu ya kupikia, bali ijishughulishe na nishati kwa upana wake kama ambavyo malengo ya kuanzishwa kwake yalivyo.

Pambazuko linaiasa REA isiishie tu kwenye nishati ya kupikia, kwani Tanzania inazo nishati za aina nyingi, ikiwemo gesi, upepo, jua, makaa ya mawe na mafuta ya aina mbalimbali kwa kutaja kwa uchache.

Ikumbukwe kuwa suala la gesi mathalan, kwa muda mrefu kumekuwa na lengo la kutaka gesi asilia itumike majumbani na kwenye magari, ingawa kuna kasi ndogo ya mabadiliko hayo.

Kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa suala hilo umekuwa ukisuasua sana. Ingawa nchi ina hazina kubwa ya gesi, inayotakiwa kutumika zaidi ili kunusuru uharibifu mkubwa wa mazingira tunaoshuhudia nchini.

Wakati Uarabuni wakiibuka na mafuta ya kuendeshea magari kutokana na mbegu za tende, ni wakati sasa wa REA nayo kuingia kazini na kuibuka na utafiti wa aina kama hiyo kulingana na mazingira yetu, hapo jambo hili likifanyika, basi REA itakuwa imetenda vyema zaidi kwa Watanzania.

NIJIPUMZIKIE MIE...



RAIS mtaafu wa Tanzania – wa awamu ya nne, **Jakaya Mrisho Kikwete**, akiwa amepumzika nyumbani kwake Kijiji cha Msoga, Wilaya ya Chalinze, Mkoa wa Pwani. (Mpigapicha Maalum).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



“Wanasiasa kuweni na ngozi ngumu kutumikia wananchi. Ni lazima kukubali mawazo ya wale unaowaongoza; wapo wenye maneno mabaya- wavumilie, wapo wenye maneno mazuri – yapokee. Yote yako.” – Samwel John Sitta, aliwahi kuwa Spika la Bunge la Tanzania. Alifariki Novemba 07, 2016.

Tangazo

Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliowaomba kuchagua, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

Mhariri Mkuu,
Oktoba, 2023

Changia Pambazuko liendelee

WAJUMBE wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufuraha kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakituma fedha, muda, ujuzi na rasilimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokuwa zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukaza Kiwahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeviza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yamevuka wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majaraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kumarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kusuzwa, lakini hasi kubaliana na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapata kuchangia maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sawa ya "asante" kutoka kwetu.

Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263

Ukitema mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandali: **Pambazuko Gazeti**. Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliowaomba kuchangia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.

Lipa kwa Simu

Lipa kwa kuscanner



Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI

 Tigo
 Safaricom
 Airtel
 Holeisima

Samia ashinde mthani wa Muungano

Na Igo AI

LEO Mzee Tai ana kitu kizito. Maana siyo kawaida yake kudamka na kuagiza lundo la magazeti ili apate habari na yanayojiri duniani.

Alipoletewa magazeti aliomba apelekewe kiti chake mbele ya nyumba ambako kuna kivuli kizuri cha mti anaodai alipanda mwenyewe.

Eti mche wa mti huo, asiojua jina lake, aliupata kutoka Entebbe, Uganda wakati akirejea nchini, baada ya majeshi ya Tanzania kumchakaza Idi Amin, Rais wa Uganda aliyefurushwa na makamanda wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWZ) kwa kuleta fujo.

Ukimya ulitawala wakati Mzee Tai akiendelea kuperuzi magazeti aliyopata. Alionekana akifungua kurasa moja hadi nyingine.

Zipo kurasa alizosalia hapo kwa muda, akionekana kutafuta taarifa Fulani, na zipo zingine, hata sekunde 59 hazifiki. Anafunika na kuendelea na zingine.

Baada ya muda kama dakika 50 hizi, Mzee Tai akamuita mwandishi wake na kuomba aletewe magazeti ya miezi miwili, Machi, Aprili ili afanye kile alichokusudia.

Magazeti yaliletwa kutoka maktaba kubwa ya vitabu na majarida anayoitunza kuliko hata mboni ya jicho kale na kuliko kitu kingine chochote. Hakuna mtu anaruhusiwa kuingia hovyoyote, na hapendi mtu akiingia achukue kitabu ama gazeti bila ruhusa yake.

Baada ya muda kupita, Mzee Tai akanyanyuka, akisikika kugugumia, kama vile mtu amepatwa maumivu ghafla.

Mzee Tai wakati anaelekea sebuleni, akamuita kijana anayemsaidia majukumu hapo ndani na kumuuliza endapo chai ilikuwa tayari. Kijana akasema ndiyo.

Mzee Tai badala ya kuketi kwenye kochi analopenda, pembeni mwa dirisha kubwa hapo sebuleni, akaelekea



Rais Samia Suluhu Hassan

chumbani kwake na huko alikaa kwa muda mrefu, hadi alipotaarifiwa na kijana wake kwamba amepata mkate kwa ajili ya kustaftahi.

Mzee Tai akatoka chumbani, lakini wakati huu alisikika akifoka tu na maneno yake hayakusikika sawasawa, kwa kuwa hutamka haraka-haraka.

“Hii nchi ngumu sana, yaani tena hawa watu wameanza mambo yao na fitna zao, kwani mama ana kosa gani, wapi ameteleza, wapi kavuruga? Iweje watu wamuibukie sasa? Yaani Mungu huyu, da! Lilalama mzee huyo mstaafu wa jeshi akiwa na miaka 71 sasa.

Akaendelea; “yaani hili suala la Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, linaonekana kuwa na agenda ya siri, tena nadhani ni zito na linahitaji mama kuwa mtulivu zaidi. Huu ni mthani wenye hila, wanachokifanya hawa watu wanajua wao, lakini namuimbea heri mama ashinde mthani huu mzito.”

Mzee Tai akamuita mwandishi wake, huku akimtaka kueleza msimamo wake kuhusu Muungano, hata kabla mwandishi wake hajatoa mtazamo, akashtukia amepigwa mbata mgongoni, huku babu huyo akitweta.

“Kawaambie hao wenzako huko kuwa huu mthani wa Muungano, mama anaushinda asubuhi sana. Subirini,” akang’aka.

Habari

Mifumo ya elimu bado kizungumkuti

Na Mwandishi WETU
Dodoma

MABADILIKO ya mara kwa mara ya mifumo ya elimu Tanzania; kuanzia elimu ya awali hadi vyo u kuu, bado yameshindwa kusaidia wananchi kujikomboa kifikra.

Haya yanabainika kutokana na nchi kuendelea kukumbwa na changamoto nyingi, ambazo zingeweza kutatuliwa na wenye elimu, lakini nao wanabaki kulalama, kama wale wa “ngumbalu.”

Imebainika kuwa kushindwa huko kunatokana na kuendelea kukumbatia mifumo inayowafanya wanafunzi kukariri zaidi masomo kwa ajili ya kufaulu mitihani, na siyo kuwa chanzo cha kumiliki uwezo wa kukabili changamoto.

Ni kutokana na hali hiyo, wiki iliyopita jijini Dodoma, mjadala mkali ulizuka bungeni baada ya kuwasilishwa kwa bajeti ya Wizara ya Elimu kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Katika mjadala huo, wabunge wengi walitaka mifumo ya elimu iliopo irekebishwe haraka kwa sababu ina kasoro nyingi zinazodumaza “bongo za wanafunzi.”

Waziri Kiongozi (mstaafu) wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mbunge wa Kuteuliwa, Shamsi Vuai Nahodha, alibainisha katika mchango wake kuwa inashangaza watoto wadogo katika shule za msingi wamerundikiwa masomo mengi ya kusoma wakati inafahamika wazi kuwa uwezo wa ubongo wa mtoto kukamata mambo kwa haraka ni mdogo sana.

Kutokana na mrundikano huo wa masomo, Nahodha alibainisha kuwa watoto wengi hawajifunzi vitu vya maana, isipokuwa kukariri wanayofundishwa kwa ajili ya kufaulu mitihani tu.

“Ukimuona mtoto wa shule ya msingi hivi sasa, utamhurumia, anabeba begi kubwa la vitabu na madaftari utadhani



Prof. Mkenda

askari anayekwenda kwenye mafunzo ya kijeshi,” alisema Nahodha na kuongeza:

Alishauri kwamba weledi ni kusoma mambo machache na kujifunza mambo mengi, siyo kusoma mengi huku ukijifunza machache.

Nahodha alishauri kuwa katika ngazi ya darasa la kwanza hadi la tatu, watoto wafundishwe masomo matano pekee ya Kiingereza, Kiswahili, sayansi, hisabati na elimu ya dini.

Baada ya hapo kuanzia darasa la tano waongezewe somo la ‘programming’ ili kuwafanya wawe sambamba na maendeleo ya kiteknolojia yanayoongoza dunia hivi sasa.

Kwa upande wake, Mbunge wa Singida Mjini, Mussa Sima, aliipongeza wizara kwa kufanya mabadiliko makubwa yaliyotangazwa na Waziri wa Elimu, Prof. Adolfu Mkenda katika hotuba yake ya bajeti, lakini alihofu kuwa utekelezaji wa mipango hiyo hautafanikiwa kutokana na ufinyu wa bajeti.

Katika bajeti hiyo, Prof. Mkenda alilambia bunge kuwa wizara anayoongoza, itaimarisha mafunzo ya amali kwa kuanzisha shule maalumu za mkondo huo.

Prof. Mkenda alibainisha kuwa kwa kuanzia zitaanzishwa shule 96, huku 28 zikiwa ni za serikali kwa ajili ya utafiti wa

Mifumo ya elimu bado kizungumkuti

Inatoka Uk. 6

awali wa program hiyo.

Hata hivyo, Sima alisema licha ya uzuri wa mpango huo, bajeti iliyowasilishwa na waziri inatia shaka kuhusiana na uwezo wa kifedha wa kutekeleza yaliyopangwa.

“Waziri ametuambia hapa kwamba wana mpango wa kujenga shule za sekondari za ufundi 100, lakini shule 26 mwakani zitaanza kupokea wanafunzi, hofu yangu hapa ni bajeti, tumeona asilimia 60.3 (ya bajeti ya wizara) inaenda kwenye mikopo ya elimu ya juu, inayobaki ndiyo tunayoipangia matumizi,” ameshangaa Sima.

Mbunge huyo akabainisha kuwa ni asilimia mbili tu imetengwa kwenye enep la elimu ya ufundi na mafunzo ya teknolojia.

“Sasa kama umeweka asilimia mbili, tumeweka shule 96 maana yake hatutafikia malengo na bado tuna shule zingine 100,” alisema.

Sima alilambia bunge kuwa bajeti hiyo ndio ilitakiwa itoe picha ya kuonyesha kweli serikali ina dhamira ya kupata vijana wenye ujuzi.

“Bajeti hii ilipaswa iweke fedha za kutosha kwenye kitengo hiki cha amali,” alisisitiza.

Mbunge huyo alisema licha ya wizara kwenda kujifunza jambo hilo katika nchi nyingine ikiwamo Ethiopia, Kenya, Rwanda na Ujerumani, lakini uzoefu kutoka Tanzania unatoa picha tofauti na yale yalioonekana katika nchi hizo.

Akifafanua, Sima alisema kuwa kulikuwa na shule nane za ufundi nchini katika miji ya Arusha, Moshi, Mbeya, Ifunda, Ihunga na nyingine nyingi, lakini hivi sasa zote hizo hazipo au zimebadilisha mwelekeo wake.

Aidha, mbunge huyo alishangazwa na hatua ya kuendelea kuiweka elimu ya msingi na sekondari chini ya usimamizi wa idaya wizarani na kwamba hiyo inafifisha elimu katika ngazi hiyo.



Bunge

“Sasa leo nataka kuja na ushauri; ushauri wangu tunahitaji hii idara iwe taasisi kama ambavyo vyiuo vikuu vina taasisi katika maeneo mahsusi yenye kipaumbele.

Mbunge huyo alifanya rejea kwenye mapendekezo ya Tume ya Jackson Makwetta ambayo ilitoa mapendekezo mazuri ya jinsi ya kuipeleka nchi kwenye uimara wa mfumo wa elimu na kuitaka serikali kurejea mapendekezo ya tume hiyo.

Katika taarifa yake, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, nayo ilieleza kuwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye wizara hiyo upatikanaji wa fedha kutoka Hazina siyo miongoni mwa changamoto za utekelezaji, bali suala la ufinyu wa bajeti kwa miradi inayopangwa kutekelezwa.

Kamati hiyo ilieleza bunge kuwa hali ya ukusanyaji wa mapato katika mwaka huu wa fedha ndani ya idara na taasisi za wizara hiyo ni wa kutilia mashaka.

“Lengo la jumla la makusanyo ya maduhuli kwa wizara hii ikiwa ni takriban robo ya tatu ya kipindi cha utekelezaji wa bajeti, lilifikiwa kwa asilimia 46 tu, ilisema kamati hiyo katika taarifa yake bungeni.

Katika bajeti hiyo bunge liliidhinisha jumla ya shilingi trilion 1.968 kwa mwaka wa fedha 2024/25 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo.

Habari

Malima aumizwa utalii Moro kuwa gizani

Na Rashid MTAGALUKA,
Morogoro

KUWEPO kwa vivutio vya utalii ukukiki mkoani Morogoro, huku waandishi wakishindwa kuvitangaza, “kumempandisha hasira” mkuu wa mkoa huo, Adam Malima.

Hasira za Malima zilidhihiri baada ya kueleza kuwa “amekuja kuwabonda” waandishi hao kwa kuwa wamepuuza kuutangaza mkoa huo wenye vivutio anuai, lakini havitambuliki kwa watu.

Malima alisema ni aibu kwa waandishi wa habari kuona masuala ya utalii ni madogo, na kung’ang’ana na habari za siasa tu kila uchao.

“Mmenialika kuja kufungua mkutano wenu wa mafunzo kuhusu namna bora ya kuandika habari za utalii, sasa mimi sitahutubia, bali nimeamua kuwabonda, kwa kuwa hata nafasi yenu na ukuu wenu hamuutambui,” alisema Malima Mei 12, mbele ya waandishi hao wa habari mjini Morogoro.

Katika mkutano huo wa mafunzo ulioandaliwa na Chama wa Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa), Malima alisema ni wakati muafaka sasa kwa waandishi wa habari wa Mkoa wa Morogoro kujikita kuutangaza mkoa huo wenye vivutio visivyopatikana popote Afrika na pengine dunia.

“Nani kati yenu anafahamu kuwa Morogoro kuna tigerfish, hakuna, sasa kama na ninyi hamjua, mtaandika nini kwa umma? Sasa ninyi Tampa tunakwenda kuwa na awamu ya pili ya mafunzo haya, na yatafanyika mbugani, huko mtapata mengi ya kuutangaza Morogoro na vivutio vyake,” aliongeza Malima.

Mkuu huyo wa mkoa aliunda kamati ya kampeni ya kutangaza vivutio vya utalii vya mkoa wa Morogoro na kwamba waandishi waliohudhuria mafunzo hayo



Mkuu wa mkoa wa Morogoro, Adam Malima.

wanakuwa wajumbe.

Alisema wajumbe wa kamati hiyo, wataandaliwa mafunzo zaidi ili kuwa na mwanga wa kutangaza vyema vivutio vya utalii vilivyomo Morogoro.

Mkufunzi kutoka Chuo cha Taifa cha Utalii, Amir Abdi, alisema licha kuwa Tanzania ina vivutio vingi vya utalii, lakini baadhi ya wanachi hawana uelewa mpana juu ya vivutio hivyo kutokana na kukosekana kwa taarifa sahihi.

Peter Nyanje, mhariri mtendaji wa gazeti Pambazuko aliwafundisha waandishi hao uandishi mzuri wa habari za utalii na kuhimiza kuwa sekta hiyo inaonekana “kulala” kwa kuwa waandishi nao wamelala.

Rais wa Tampa, Simon Mkina akizunguzia lengo la mafunzo hayo yaliyoandaliwa kwa ufadhili wa Shirika la Hifadhi ya Taifa (Tanapa) kwa kushirikiana na Gazeti Pambazuko, ni kutoa fursa kwa waandishi kupata mafunzo sahihi ya namna kutangaza vivutio vya utalii kwa kila mkoa.

Kabla ya mafunzo hayo yaliyowakusanya waandishi 40 wa Morogoro, Mkina alisema Tampa imewezesha mafunzo kama hayo kuwafikia baadhi ya waandishi wa Dar es Salaam, huku wanahabari wa mkoa ya Mwanza, Njombe na Kilimanjaro wakitakiwa kujiandaa kwa mafunzo kama hayo.



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

‘Wadudu’ Arusha vs ‘Komandoo Yosso’ Dar

Na Rashid MTAGALUKA

‘MAKUBALIANO’ kati ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda na kikundi cha vijana wanaodaiwa kuwa wezi, vibaka na wakwapuaji; wanaotumia vitu vyenye ncha kali kama visu, kupora – kwamba sasa “wanakuwa walenzi wa amani” ni jambo la kupongezwa.

Napongeza makubaliano hayo kwa sababu ni nadra kwa vikundi kama hivi vinavyosifika kwa matukio ya uporaji na uvunjifu wa amani, kujitokeza hadharani mbele ya mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama wa mkoa.

Makonda anasema kuwa amekubaliana na vijana hao sasa kulinda mkoa mzima na wakazi wake kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, viongozi wa dini na serikali.

“Mheshimiwa Makamu wa Rais, naomba nitangaze rasmi Arusha ni shwari na ni sehemu salama sasa ya kuishi, kwani wale vijana waliokuwa wanaogopeka maarufu kama wadudu, sasa hawang’ati tena maana tumekula nao kiapo usiku huu wa leo pale karibu na ofisini kwangu - cha kulinda mkoa wetu na watu wake” alisema Makonda.

Kwa kweli sijui na wala sitaki kuhoji kama katika kipindi chote cha ‘wadudu’ kung’ata Arusha hakukuwahi kuripotiwa tukio lolote la uporaji kwenye vituo vya Polisi na waathirika wa matukio hayo wamemalizanaje na kikundi hiki cha wahuni baada ya ‘kukumbatiwa’ na wenye mamlaka!

Kwamba anajisikiaje aliyeporwa pipikipi, pesa, simu yake na kujeruhiwa na ‘Wadudu’ wa Arusha, leo akiwaona watesi wake wakikata keki na kupiga picha na mkuu wa mkoa!

Kwa wale wenye kumbukumbu za



Paul Makonda

miaka ya 1990, watakukubaliana nami uwepo wa kikundi maarufu cha vijana wadogo wahalifu kama hicho jijini Dar es Salaam kilichojiita ‘Komandoo Yosso’.

Kikundi hiki ambacho kilikuwa kikivamia mitaa mbalimbali ya jijini la Dar es Salaam na kufanya uhalifu wa kupora kwa kutumia silaha za jadi pamoja na kuvunja nyumba, kilitishia amani na usalama wa wananchi kwa kiasi kikubwa.

Miaka hiyo ukirudi kazini usiku ni mashaka matupu! au kwenda kuangalia mnanda/mchiriku ilikuwa mwisho saa moja usiku, zaidi ya hapo lazima lazima kuomba msaada wa Polisi.

Sikumbuki vikundi hivi vilidhibitiwaje, lakini vilikuwa vikundi hatari, na kwa hatari hiyo jamii ya watu wenye hasira kali iliamua kumalizana nao huko huko mtaani kwa kuwachoma moto baada ya kuwakamata.

Hata hivyo, uwamuzi wa mchawi kumpa mwana alee ni nzuri maana huko nyuma hatukuwahi kushuhudia gavana yeyote wa Dar es Salaama akivaa ujasiri wa kupiga picha na Komandoo Yosso, Mbwa mwitu au Panya road.

•Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari anapatikana kwa simu namba 0784 438546

Barua pepe:mtagaluka@gmail.com

Kenya

Nyota ya mwanajeshi mwanamke yang'ara

Na Julius MKAMBI,
Nairobi

MIKAKA sita iliyopita, Rais (mstaafu) wa Kenya Uhuru Kenyatta aliweka historia pale alipomteua mwanamke wa kwanza kuwa brigedia kisha akampandisha cheo kuwa Meja Jenerali wa Jeshi la Ulinzi la Kenya (KDF), na sasa nyota ya mwanajeshi huyo wa kike inazidi kung'ara.

“Ni fahari na furaha yangu kumtambulisha mwanamke wa kwanza Mkenya kuwa Meja Jenerali katika jamhuri yetu. Nakutegemea wewe uwe mfano wa kuigwa na wanawake humu nchini na kuwathibitishia hakuna kikomo kwa wanawake wa Kenya,” alisema Rais Uhuru wakati akitangaza uteuzi wa Fatuma Gaiti Ahmed kuwa msaidizi wa aliyekuwa Mkuu wa Majeshi, Samson Mwatethe.

Hakika Meja Jenerali Fatuma anazidi kuwa mfano wa kuigwa, hususan na wanawake baada ya Rais William Ruto mapema mwezi huu kumpandisha cheo na sasa anakuwa Kamanda wa Kamandi ya Wanaanga.

Uteuzi huo wa Fatuma ulienda sanjari na uteuzi wa Mkuu wa Majeshi, Charles Muriu Kahariri, ambaye anaziba pengo lililoachwa na Jenerali Francis Ogolla aliyefariki kwenye ajali ya ndege pamoja na wanajeshi wengine tisa.

Kahariri ambaye awali alikuwa Makamu wa Mkuu wa Majeshi akishikilia cheo cha Luteni Jenerali, sasa amekuwa Jenerali.

Meja Jenerali John Omenda anayeongoza tume inayochunguza kifo cha Jenerali Ogolla, amepandishwa cheo cha Luteni Jenerali na kuteuliwa Makamu wa Mkuu wa Vikosi vya Ulinzi Kenya.

Awali, Luteni Jenerali Omenda alikuwa Kamanda wa Kamandi ya Wanaanga, nafasi ambayo sasa inamwendea Meja Jenerali Fatuma, huku Rais Ruto akimteua



Fatuma Gaiti Ahmed

Meja Jenerali Paul Owuor Otieno kuwa Kamanda wa Kamandi ya Wanamaji.

Hata hivyo, ni uteuzi wa Meja Jenerali Fatuma ndiyo ulikuwa gumzo ikizingatiwa anaweka historia ya kuwa mwanamke wa kwanza kushikilia wadhifa huo katika Vikosi vya Ulinzi vya Kenya.

Cha kushangaza ni kwamba safari ya uwanajeshi ya Meja Jenerali Fatuma aliyezaliwa mwaka 1965, ilianza kimiujiza kwani alipohitimisha masomo yake ya sekondari - mwaka 1983, alikumbana na zoezi la kuajiri wanajeshi alipokuwa anasaka kitambulisho chake cha kitaifa.

Aliamua kujaribu bahati yake na kwa mshangao alichaguliwa kujiunga na jeshi na kujiandikisha katika Chuo cha Kijeshi cha Kenya kama ofisa cadet mwaka 1984 na akateuliwa kuwa Luteni wa Pili katika Jeshi la Wanahewa la Kenya mwaka uliofuata.

Upambanaji wa Meja Jenerali Fatuma kwenye taaluma yake ya uwanajeshi ni ushahidi wa udhabiti na uwezo wake na pia anaendelea kuwa kielelezo kwa wengi, akithibitisha kwamba kwa kujitolea na fursa zinazofaa, vikwazo vinaweza kuvunjwa.

Majukumu yake ya uongozi na jinsi anavyopandishwa vyeo ni jambo la kihistoria nchini Kenya, na mwanga kwa wanawake kujituma zaidi na wanaweza kufanikiwa.

Biden anabaki au Trump anarudi Ikulu?

Golden Matonga,
Phoenix

KATIKA ofisi ya uchaguzi ya Kaunti ya Maricopa, Arizona, Marekani, kamera za video hufanya kazi saa 24, zikitangaza moja kwa moja kwenye kurasa zake za mitandao ya kijamii, ikiwamo Facebook.

Matangazo yote yanayoonekana na kusikika, ni kuhusu mchakato wa kupatikana kwa Rais wa Marekani, pamoja na wawakilishi wengine wa wananchi katika ngazi za uamuzi.

Baadaye mwaka huu, hasa Novemba, wananchi wa Marekani watakuwa wakitumia haki yao ya kidemokrasia kuchagua viongozi wao wa kisiasa, akiwamo kiongozi mkuu; rais.

Mmoja - kati ya rais wa sasa wa nchi hiyo, Joe Biden na mpinzani wake, Donald Trump, lazima ataubuka kidedeo, maana hawa ndiyo wagombea wenye nguvu.

Katika uchaguzi mkuu wa nchi hiyo uliofanyika mwaka 2020, Trump kutoka chama cha Republican alidondoshwa na Biden, wa chama cha Democrat.

Ushindi wa Biden, kumuondoa Trump Ikulu kulimfanya kuamini kwamba alishindwa kwa hila, hivyo, hakutaka kutoa ushirikiano mkubwa wakati wa kukabidhi Ofisi Kuu ya Ikulu.

Trump, hadi leo anaamini alifanyiwa fitna na figisu na mpinzani wake, Biden akishirikiana na wapambe wake. Anachokiamini ni kuwa vifaa vilivyotumika kwenye mchakato mzima wa uchaguzi, 'viliharibiwa' ili kumpa ushindi mpinzani wake.

Ni kutokana na imani yake kuwa aliibiwa kura zake za ushindi, Trump na timu yake ya wanasheria wabobezi, alikimbilia mahakamani ili "kupigania ushindi wake."

Hata hivyo, pamoja na kuwa na wanasheria mahiri, na kuwasilisha nyaraka za kile walichodai uthibitisho wa ushindi wa mteja wake, waliangukia pua. Hoja za Trump hazikuweza kushawishi



Donald Trump

mahakama kupindua matokeo.

Sasa Trump anadai kurejea kwenye kinyang'anyiro akiwa na nguvu mpya na maarifa ya kuhakikisha anamuondoa Biden madarakani.

Biden na wafuasi wake, nao wanatamba kwamba mpinzani wao kamwe hawezi kurejea Ikulu kwa kuwa "alivuruga" mambo mengi na kusababisha maisha magumu kwa idadi kubwa ya watu.

Timu ya Biden, inadai kuwa Trump wakati akiwa madarakani, alipelelea zaidi wafanyabiashara wakubwa na matajiri, kwa kuwa ndiyo kundi lake, na kuwasahau watu wa hali ya kati na wale wenye hadhi ya chini.

Tayari kampeni za uchaguzi huo zimeanza na zinashika kasi kila uchao.

Trump na Biden wanafanya kampeni dhidi ya kila mmoja wao, tena - na - tena, uaminifu wa uchaguzi unashambuliwa, na wachambuzi wengine wakihoji kuwa Trump tayari anaweka msingi wa kudharau matokeo ikiwa atashindwa.

Pamoja na pilikapilika za wagombea hao, mwamuzi ni sanduku la kura na kutangazwa kwa matokeo halali.

Makala haya yametafsiriwa kutoka gazeti la The Continent linalochapishwa kwa lugha ya Kiingereza.

Afya**Lupus haiambukizi. Wagonjwa wasaidiwe**

Na Mwandishi WETU

MARA nyingi binadamu huingiwa woga wanapotambua kuwepo kwa magonjwa yasiyofahamika zaidi.

Hofu hutanda zaidi sana baada ya watu - wasiokuwa wataalamu wa afya, kuanza kusambaza mengi ya kuogofya, wao wakidhani wanahadharisha jamii, kumbe wanajaza hofu bila sababu.

Miaka ya hivi karibuni, kumekuwapo ongezeko la watu wanaobainika kuwa na ugonjwa wa Lupus.

Ugonjwa huu haukuwa ukifahamika kwa wengi kutokana na kuwepo kwa wagonjwa wachache.

Lakini, ongezeko la watu, kumeibua idadi inayoongezeka ya wagonjwa wa Lupus, wanaobainika baada ya kufanyiwa uchunguzi wa afya kwenye hospitali kubwa.

Baadhi yao wamekuwa wakiwanyapaa wagonjwa wa Lupus kwa hofu ya kuambukizwa, lakini ukweli uliothibitishwa na madaktari, ni kwamba Lupus haiambukizi kutoka mtu mmoja kwenda kwa mwingine.

Matabibu wanaeleza kuwa Lupus ni ugonjwa unaoshambulia mfumo wa kinga ya mwili, hasa maeneo ya tishu na viungo vyake pamoja na kuathiri baadhi ya sehemu mbalimbali ikiwemo ngozi, figo, mapafu, moyo, seli za damu, ubongo, na mifumo mingine ya kisaikolojia.

Ugonjwa huu hauna dalili za moja kwa moja, hivyo ni ngumu kujulikana haraka kwani dalili zinatofautiana kulingana na sehemu ya mwili iliyoathirika.

Hospitali ya Medcover, ya India, kupitia toviti yake, inaeleza dalili za awali za ugonjwa wa Lupus kuwa ni pamoja na uchovu wa mwili usiokuwa na sababu maalum, homa inayoongeza zaidi joto la mwili na maumivu ya viungo.

Dalili zingine ni ngozi kuwa na vidonda vidogo vidogo, huku vidole vya mikono, kugeuka kuwa vyeupe au bluu wakati wa baridi.

*Moja ya dalili za Lupus*

Pia mgonjwa wa Lupus hupata shida kwenye mfumo wake wa kupumua, kupata maumivu ya kifua, macho kuwa makavu na maumivu ya kichwa.

Tukomeshe kunyanyapaa

Kuwepo kwa matukio ya kunyanyapaa wagonjwa wa Lupus, kumemuibua Mkurugenzi wa Huduma za Tiba Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dkt. John Rwegasha ambaye ametoa rai kwa watu kuacha kuwatenga kwa njia yoyote wagonjwa wa Lupus.

Akizungumza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ugonjwa wa Lupus ambayo huadhimishwa kila Mei 10 – ya kila mwaka, amesema “hakuna sababu ya kuwanyanyasa na kuwanyanyapaa wagonjwa wa Lupus.”

Naye daktari bingwa wa magonjwa ya ngozi Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dkt. Andrew Foi amesema ugonjwa huo unawapata watu wa rika zote na wanaoathirika zaidi ni wenye umri kuanzia miaka 31 hadi 40.

Dkt. Foi ameeleza kuwa tafiti zinaonyesha wanawake ndio wanaoathirika zaidi na ugonjwa huu kuliko wanaume.

“Kwa mwaka 2022 /2023 wagonjwa 101 waliandikishwa katika kliniki zetu Muhimbili, ambapo kati yao wanawake walikuwa ni asilimia 86,” amesema Dkt. Foi.

Biteko afunda viongozi wa wilaya

Na Mwandishio WETU
Dodoma

WAKUU wa wilaya, makatibu tawala na wakurugenzi wa halmshauri nchini, wametakiwa kufahamu kuwa ulinzi wa amani na utulivu nchini ni dhamana wanayoibeba.

Hayo yameelezwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt. Doto Biteko wakati akifungua warsha iliyowaleta pamoja viongozi hao kutoka mikoja tisa ya Tanzania Bara kuhusu usimamizi na utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai iliyofanyika jijini Dodoma karibuni.

Dkt. Biteko aliwaambia viongozi hao kuwa ulinzi wa amani na utulivu nchini unaanza na wao kwani wao ndiyo nguzo ya kupatikana kwa haki jinai katika jamii.

“Wakuu wa wilaya, makatibu tawala na wakurugenzi dumisheni amani na mshikamano katika maeneo yenu ya kazi na kati yenu na wananchi ili kujenga taswira nzuri,” alisema.

Dkt. Biteko alisema inasikitisha kuona kuwa baadhi ya viongozi wanaopaswa kufanya kazi pamoja kwa kushirikiana, hawaelewani, hivyo kusabisha migogoro mahali pa kazi na pengine kusababisha hasara kwa serikali.

Alihoji iwapo viongozi hawataelewana je, watawezaje kuwaleta wananchi pamoja?

Naibu waziri mkuu huyo alisisitiza umuhimu wa viongozi kutekeleza majukumu yao na kufanya uamuzi kwa kuzingatia sheria na miongozo iliyowekwa, kushirikiana na taasisi za haki jinai na kujipanga kutekeleza mkakati wa kubaini uhalifu kabla hajatendeka badala ya kusubiri utokee ndipo wakabiliane nao.

“Wekenzi mkakati thabiti wa kuzuia migogoro ya ardhi na endeeleni kuweka utaratibu wa kusikiliza kero za wananchi na kuzifanyia kazi kwa kuzingatia sheria.



Dkt. Doto Biteko

Tatueni kero za wananchi kwa haki bila kumuonea mtu”, alisisitiza.

Awali, akitoa maelezo kuhusu matokeo ya Tume ya Haki Jinai, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Tume ya Haki Jinai, Inspekta Jenerali wa Polisi (mstaafu), Said Mwema, alisema kuwa ripoti hiyo inaonyesha kuwa wananchi wamekuwa na maoni mbalimbali ikiwemo malalamiko.

Alisema malalamiko mengi yalihuwa huduma duni, ukosefu wa maadili, vitendo vya rushwa na migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji na wananchi na taasisi za serikali pamoja na ukamataji wa watuhumiwa bila kuzingatia utaratibu wa haki zao za msingi.

Baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Haki Jinai tayari yameanza kufanyiwa kazi na serikali. Moja kati ya mapendekezo yaliyofanyiwa kazi ni kufunguliwa kwa ofisi 50 za mkurugenzi wa mashitaka katika ngazi ya wilaya nchini ili kusaidia upatikanaji wa haki nchini.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan aliunda tume hiyo mwezi Januari, 2023 ikiwa na wajumbe tisa na kuipa kazi ya kupitia na kutoa mapendekezo ya kuboresha mfumo wa taasisi za haki jinai nchini kazi iliyokamilika na taarifa yake kuwasilishwa Julai, 2023.

Je, unafahamu hii?

Kondomu zenye miiba 'kiboko' ya wabakaji

ONGEZEKO la matukio ya kubaka huko Afrika Kusini, kuliubua ubunifu wa kondomu zenye miiba ili kubaini na hatimaye kukamata wabakaji.

Kinachofanyika ni kwamba mwanamke anayehisi kuwepo kwenye mazingira ya kubakwa, huiingiza ukeni na endapo kweli mbakaji atamvamia, basi, hutoa ushirikiano, ili asiawe wala kuumizwa.

Sasa basi, mbakaji anapomaliza 'shughuli' yake huondoka juu ya mwili wa mwanamke huyo huku kondomu ikinasa kwenye uume wake.

Miiba hiyo huzuia kondomu kuvuliwa kwa kuwa hunasa kwenye ngozi ya uume wa mbakaji na hawezi kuivua kwa kuwa miiba hunasa na kuumiza zaidi kila anapolazimisha kuitoa.

Dawa ni kwenda hospitali kwa ajili ya kuiondoa kitaalamu na hapo polisi huitwa kumkamata mbakaji na sheria kuchukua mkondo wake.



Kondomu yenye miiba

Hatua hii imesaidia mno kupunguza janga la ubakaji Afrika Kusini na kondomu hiyo sasa imesambazwa nchi kadhaa duniani.

Mbunifu wake, Sonette Ehlers, amepokea tuzo kadhaa duniani kwa uvumbuzi huu na ameruhusu viwanda kadhaa kuanza kuzitengeneza kwa wingi ili kuokoa wanawake kubakwa na kusababisha magonjwa, ikiwamo ukimwi na mimba zisizotarajiwa.

Tarehe maalum ya kutia mimba

HALJAELEWEKA hadi sasa kwanini Warusi (Warussia) hawapendi kuwa na watoto.

Wapo wanaodai ni kutokana na maisha magumu, wengine wakieleza ni staili ya maisha; ambapo vijana wengi wanapenda kutumia muda wao kufanya kazi na starehe na siyo kulea.

Vyovyote iwavyo, Warusi wamekuwa wagumu kutengeneza familia kubwa. Wanawake wanapenda kuishi peke yao, kama ilivyo kwa wanaume.

Wakiamua kuoana, basi hukubaliana kutokuwa na watoto, kwani wanataka kufanya kazi zaidi na kutumia muda mwingi kustarehe. Wanadai, "maisha yenyewe mafupi."

Staili hii ya maisha imekuwa ikiwastaajibisha wazee na kuanza kulalamika kwa serikali.

Mwaka 2006, Rais wa Russia, Vladimir Putin alisikia kilio cha wazee, hasa

wanawake na mikakati ya kuhamasisha vijana kupata watoto.

Hivyo, akatangaza kuwepo kwa tarehe maalum ya wananchi wake, wanaume, kutia mimba wenza wao; iwe wameoana au kuwepo kwa makubaliano ya kisheria.

Katika kampeni hiyo ya kuhimiza vijana kuongeza familia, Rais Putin akaitaja Septemba 12 kila mwaka kuwa siku muhimu ya wanaume kutia mimba wenza wao.

Mbali na tarehe, pia akatangaza kuwepo kwa motisha, kwamba familia itakayoamua kupata mtoto itapewa fedha, pia ile yenye kuamua kuongeza mtoto, itaifaidika kwa fedha taslim na baadhi ya matibabu ya mtoto bure.

Ikawa rasmi kwamba Septemba 12, ya kila mwaka ni siku ya mapumziko, huku ikihimizwa kuwa wenza wafanye kazi moja tu; kufanya mchakato wa kupata mtoto.



Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au
Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Matukio katika Picha



Rais wa Tanzania Samia Suluhu Hassan akizungumza jambo na mtoto Khaira Ali Jabir mara baada ya kuwasili Jijini Paris, Ufaransa kwa ajili ya kushiriki Mkutano wa Kimataifa wa Nishati Safi ya Kupikia. Rais Samia na timu yake waliwasili huko jana - Mei 12. (Picha na Ikulu)



Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Afrika Mashariki (TAEF), Churchill Otieno (kulia), akifurahia jambo na mwandishi mkongwe kutoka Ghana, Emmanuel Dogbevi. Manguli hawa walikutana hivi karibuni jijini Accra, Ghana. (Picha kutoka mtandao).



Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima (Katikati) akizungumza jambo katika ufunguzi wa mafunzo ya namna ya kuandika vyema habari za utalii kwa waandishi wa habari. Mafunzo yalitanyika Mei 10, 2024 mjini Morogoro. Kulia ni Rais wa Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa), Simon Mkina na kushoto ni Katibu Mtendaji Chama cha Waandishi wa Habari Morogoro, Lilian Lucas. (Picha na Juma Mtanda).

MCT kuziba ombwe habari za uchaguzi

Na Simon Mkina

THAMANI na umuhimu wa vyombo vya habari kwa maendeleo ya nchi, ustawi wa haki na makuzi ya demokrasia, haubishianiwi hata kidogo.

Hakuna anayeweza kupinga mchango wa vyombo vya habari kwenye kila mafanikio ya nchi. Hata pengine, jumua na mtu mmoja mmoja.

Hata hivyo, pia mchango wa vyombo vya habari unaweza kuwa hasi ikiwa vitatumika ama kutumiwa vibaya, ingawa hili limekuwa na mjadala mpana. Kwamba hili likitokea, maana yake kuna kukengeuka kwa chombo husika.

Kitokea mchango wa habari ukawa hasi, basi lazima kuna kutofuatwa kwa maadili na weledi wa taaluma utakuwa umewekwa pembeni.

Weledi na maadili ya uandishi wa habari unapasswa kusimamiwa kwa wivu na kwamba vyombo vya habari vinapaswa kuwa na heshima, kama ilivyo kwa mihimili mingine mitatu ya utawala; serikali, mahakama na bunge.

Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni, vyombo vya habari nchini Tanzania, vimeingia katika tuhuma za kuandika ambazo hazisaidii zaidi nchi na jamii iliyomo.

Kwamba vyombo vya habari vimejikita zaidi kuandika na kutangaza habari zinazohusu “porojo zaidi” – kwa maana ya kuandika habari za watu binafsi na kuacha kufuatilia na kuandika masuala yanayosaidia nchi.

Hali hiyo iko kwenye maeneo mengi; lakini linaloumiza na kuleta mazingira ya kuminya haki, ni katika mchakato wa kupatikana kwa demokrasia – kupitia sanduku la kura; uchaguzi.

Katika uchaguzi wa Tanzania, imebainika kuwa vyombo vya habari vimeacha kuandika masuala, ili kuwapa wapigakura haki ya kuwa na uchaguzi wenye manufaa, bali vinaandika zaidi matukio na wagombea.

Hiyo inadhahirisha kuwepo kwa ombwe, linalohitaji nguvu ya zaida



Katibu Mtendaji wa MCT, Ernest Sungura

kulijaza kwa njia ya kupigania vyombo vya habari kuandika masuala.

Hali hiyo imekuwa ikishtua na kulalamikiwa na idadi kubwa ya wananchi, hivyo kuhitaji taasisi ama ofisi kufuatilia na kujikita kuhakikisha vyombo vinafanya majukumu yake makubwa kwa kusaidia nchi kwa kuandika habari za masuala.

Baraza la Habati Tanzania (MCT), kutokana na ombwe hilo, limeamua kufanya kazi ya kuhakikisha vyombo vya habari vinajikita kuandika habari za masuala – wakati wa uchaguzi, zitakazosaidia nchi.

MCT imesema kuwa endapo vyombo vya habari vitaandika habari za masuala, vitachochea uwepo wa amani, utulivu na kuaminiana miongoni mwa Watanzania wakati wa mchakato wa uchaguzi ujao.

Katibu Mtendaji wa MCT, Ernest Sungura aliwahakikishia Watanzania kuwa baraza analoongoza litafanya kila linalowezekana kusaidia vyombo vya habari na waandishi wake kupata elimu, na ikiwezekana, uwezeshi katika rasilimali fedha ili kupata nyenzo za kufanya kazi kwa ufanisi wakati wa kuhakiki wapiga kura, kampeni, kupiga kura na kutangazwa matokeo.

“Tumeshuhudia mara nyingi wakati wa uchaguzi, vyombo vingi vya habari vinaandika kuhusu wagombea na kuacha kabisa masuala muhimu yanayogusa wananchi, hii inachangiwa

Makala**Bunge: Serikali inahujumu kilimo***Inatoka Uk. 17*

na mambo mengi, sasa MCT inajipanga kuhakikisha mchango wa vyombo vya habari unaonekana na kuthaminiwa kwa umma,” alisema Sungura katika kongamano liliandaliwa na MCT na kufadhiliwa na Ubalozi wa Marekani hivi karibuni jijini Dodoma.

Tanzania itakuwa na uchaguzi wa Serikali za Mitaa baadaye mwaka huu na uchaguzi mkuu mwaka kesho, 2025.

Sungura alisema MCT itahakikisha inatoa elimu mahsusi kwa waandishi wa habari kabla ya uchaguzi wa mwaka huu na baadaye mwaka kesho, kuhusu uelewa mpana wa sera za kila chama na kuzifafanua kwa urahisi ili zisambae kwa wananchi na wapate fursa ya kuchagua viongozi wanaowataka.

“Vyombo vingi vya habari havina mpango kazi wa masuala ya uchaguzi, hili nalo tumeona ni mihumu na tutaweza kutoa mafunzo, kwa kutumia wazoefu, ili kila chombo cha habari kiwe kinatambua kinafanya kipi, muda gani, kwa minajili ya nani,” aliongeza Sungura.

Sungura alisema vyombo vya habari vikikumika vyema kuandika, kutangaza na kuonyesha habari kwa weledi; haki, usawa na utu, ni hakika kuwa Tanzania itakuwa na uchaguzi wenye haki.

“Uandishi wa habari za uchaguzi kwa weledi, hujenga usawa, haki na uwajibikaji, na hapo ndipo tunataka mchango wa vyombo vya habari ufikie,” alisema katibu huyo mtendaji wa MCT.

Katika kongamano hilo lililofanyika Aprili 30, Jaji Joseph Sinde Warioba, waziri mkuu mstaafu, aliviasa vyombo vya habari kusaidia taifa kwa kufanya tafiti zitakazoisaidia serikali kutoa uamuzi wa kuendeleza nchi.

Warioba, ambaye pia ni makamu wa kwanza wa rais mstaafu, alionyesha kushangazwa na vyombo vya habari sasa kuandika na kutangaza zaidi habari za matukio bila kuwa na habari za kuelimisha.

Aliwataka wanahabari wasiwe sehemu ya kulalamika wakati wana nafasi kubwa

*Upigaji kura*

ya kutengeza agenda kwa kufanya tafiti na kutoa elimu ya mambo ya msingi kwa nchi.

“katika kipindi cha uchaguzi vyombo vingi vya habari vimekuwa vikiripoti na kutangaza habari kuhusu wagombea pekee na kuwanyima nafasi wapiga kura kuanzia hatua ya awali ya wandikishaji wa wapiga kura hadi kutangazwa kwa matokeo hali ambayo inachochea uvunjifu wa amani kipindi cha uchaguzi,” alisema Jaji Warioba

Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, naye ameona ombwe kwenye uadishi wa habari za uchaguzi, na kuasa waandishi kuhakisha wanaandika kuhusu masuala ili kusaidia wapigakura kuwa na uamuzi sahihi kwenye sanduku la kuchagua wawakilishi wao.

“Nawasihi waandishi wa habari kuacha kutumika katika kipindi cha uchaguzi, na badala yake kutumia kalamu zao vyema, kufichua maovu kipindi cha uchaguzi ili kuwa na demokrasia yenye haki na usawa,” aliongeza Zitto.

Zitto anasema endapo vyombo vya habari vitaamua kuwabeba wagombea wasiokuwa na uwezo wa kuongoza wala kusaidia nchi, basi, jamii itakosa mtetezi.

“Hakuna mtetezi wa wananchi kama waandishi wa habari, ambao wanawajibua mkubwa wa kuibua rushwa, kukiukwa kwa sheria na taratibu za uchaguzi, hivyo watende kazi zao kwa uaminifu na Tanzania, itapona,” ameingezwa Zitto.

Makala haya yalichapishwa kwa mara ya kwanza na gazeti la MwanaHalisi. Yanarejewa hapa kwa umuhimu wake.

Wasanii Z'bar washutumu kutelekezwa

Na Mwandishi WETU,
Zanzibar

WASANII wa fani ya uigizaji – filamu, Zanzibar wameilaumu serikali kwa kuwatelekeza, huku wakitaka kuwepo mpango mkakati wa mabadiliko utakaofanya sekta hiyo kuwa sehemu ya kukuza uchumi kwa taifa.

Kwenye mkutano wa majadiliano uliowapa nafasi adhimu ya kubadilishana mawazo juu ya namna ya kukuza sekta ya filamu Zanzibar, wasanii hao wameanza kwa kauli ya kuilalamikia serikali kupuuzwa sekta hiyo.

Wakati wakipeperusha pongenzi nyingi kwa Tamasha la Kimataifa la Filamu Zanzibar (ZIFF), pamoja na Taasisi ya Emmerson (EF), kwa kuwa msaada mkubwa, wametamka wazi kuwa “viongozi na serikali yao hawana msaada wowote kwetu.”

ZIFF ni asasi binafsi iliyoanzishwa na wazawa wakisaidiana na wadau mchanganyiko wa filamu kutoka pembe kadhaa za dunia na kila mwaka huandaa mkusanyiko unaoleta maelfu ya wasanii wakiwemo wabobezi katika utengenezaji maudhui, watunzi, waandishi pamoja na waongozaji filamu, wanasifiwa kwa kutoa mchango wa angalau kutoa jukwaa la wasanii kujinafasi.

Na taasisi ya Emmerson, iliyoasisiwa na raia wa Marekani aliyehamia Zanzibar miaka ya mwanzo ya 1990, kwa tiketi ya kuwekeza kwenye sekta ya utalii, inasaidia wasanii ikiwemo kuanzisha tuzo ya kila mwaka ya kutunuku wasanii bora wa filamu.

Lakini pamoja ya jitihada zao hizo, wakuu wao wmeshuhudia malalamiko kuwa mchango wao haujatosheleza kufikia kujenga sekta ya filamu kuwa uchumi mkubwa unaonufaisha wasanii na kuingiza pato serikalini.

“Sanaa imekwama Zanzibar, haikui kwa sababu hatuna soko la nyumbani. Sanaa kwetu ni tofauti na wenzetu Tanzania Bara ambao wanapata pesa kwa kutengeneza filamu, sisi tutafute pesa ili kutengeneza filamu,” amesema Mwenenu Mjasiri.

Jesca Christopher Mtui aliyehamia Zanzibar kutoka Bara amesema alichojifunza Zanzibar ni kwamba filamu yake haifiki mbali kwa sababu haijulikani nje - inaishia tu Zanzibar.

Mtui anasema wakati anazonia talanta za filamu, haoni mpango mahsusi wa kuzikuza. “Utakuta tunaiga utungaji wetu uwe kama wazungu. Yapo maeneo tele ya kutengeneza filamu za kiwango cha kimataifa, lakini hayatumiki na kunakosekana ubunifu.

“Tuna upungufu mkubwa wa kubuni mifumo ya kutengeneza filamu nzuri, matokeo yake kila nafasi unajikuta upo mwenyewe. Huu siyo utaratibu wa kukuza filamu, lazima kuwe na mabadiliko,” amesema.

“Elimu ya kiufundi na kule kutambua namna bora ya kutengeneza filamu kama biashara kubwa, kunahitaji iwepo sera ya taifa ya filamu na siyo kuwa suala la kubahatisha,” anasema Joseph Sumary aliyekuja Zanzibar kutafuta fursa za kutengeneza filamu.



Mama ni mhimili...



Jana, ikiwa ni Jumapili ya pili ya Mei, dunia ilisherehekea Siku ya Mama Duniani. Hakika siku hiyo hukumbusha binadamu wapi wametoka. Ni nafasi nzuri ya kurejesha amani, furaha na upendo kwa mama. Hakuna cha kumlipa mama, lakini yatosha tu kushukuru. Picha hii imechotwa kwenye mtandao wa intaneti na haikujulikana imepigwa lini, na nani na kutoka wapi.

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (TAMPA) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa msunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

